



# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com



## MATANGAZO: DOMINIKA YA 2 YA KWARESIMA A - TAREHE 01.03.2026

1.	LEO DOMINIKA 01.03.2026	<b>DOMINIKA YA 2 YA KWARESIMA MWAKA A</b> Mchango wa Pili ni kwa ajili ya Ujenzi
2.	IJUMAA 06.03.2026	Njia ya Msalaba saa 10:30 jioni ikiongozwa na VIWAWA na itafuatiwa na Misa Takatifu. Kwa kipindi cha Kwaresma, siku za Ijumaa hakutakuwa na Misa za asubuhi. Matoleo kipindi cha Kwaresma ni kwa ajili ya Kampeni ya Kwaresma
3.	JUMAMOSI 07.03.2026	Kumbukumbu ya Watalatifu Perpetua na Felisita, Wafiadini Ni Jumamosi ya Kwanza ya mwezi, Misa kwa heshima ya Moyo safi wa Maria itaadhimishwa Parokiani saa 03:00 asubuhi.
4.	DOMINIKA 08.03.2026 <b>DOMINIKA YA ZAKA</b>	<b>DOMINIKA YA 3 YA KWARESIMA MWAKA A</b> <b>Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi</b> Wasimamizi: Mt. Secilia Watangaza Neno: Angela Komba na Frank Mbowe <b>Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhu</b> Wasimamizi: Mt. Theresia wa Avila Watangaza Neno: Jackline Makondo na Pius Laswai <b>Misa ya 3: Saa 5:00 asubuhi</b> Wasimamizi: Mt. Secilia na Mt. Theresia wa Avila <b>Mchango wa pili kwa ajili ya ujenzi.</b>
5.	VIWAWA	<b>HIJA YA VIJANA JIMBO:</b> Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam Henry Mchamungu anawaalika Vijana wote kushiriki katika Hija ya Vijana Jimbo itakayofanyika 07.03.2026 katika kituo cha Hija Pugu kuanzia 02:00 - 10:00 jioni. <b>Mtukio:</b> Njia ya Msalaba, Semina, Maungamo na Misa Takatifu. Kila Jumuiya inaombwa kuchangia kiaasi cha 20,000 kwa ajili ya vijana wawili.
6.	SEMINA YA VIJANA	Kutakuwa na Semina kwa vijana wote wa Kidato cha nne Dominika ijayo 08.03.2026 mara baada ya Misa ya kwanza Dondoo 1. Stadi za bustani na maisha 2. Kujenga tabia 3. Elimu ya afya na afya ya akili

		4. Maandalizi ya kidato cha tano na chuo
7.	UCHAGUZI WA KAMATI TENDAJI	Uchaguzi wa Kamati Tendaji Parokia utafanyika Dominika ya leo 01.03.2026 mara baada ya Misa ya Kwanza. Wahusika ni viongozi 5 wa Kamati Tendaji wa Jumuiya na wenyeviti wa VMJ ngazi ya Parokia. Tunaalikwa kuendelea kusali ili kupata viongozi wa Parokia yetu.
8.	GAZETI LA TUMAINI LETU	Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5.

### **TANGAZO LA DARAJA YA UPADRI KWA MARA YA KWANZA**

Mhashamu Sana Askofu Mkuu Jude Thaddeus Ruwa'ichi OFMCap wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam anatangaza Daraja ya upadri wa Shemasi Peter Maksensius Mtendavema, SDS wa Shirika la Mungu Mwokozi - Wasalvatoriani (The Society of the Devine Savior) anayefanya uchungaji kwa sasa katika Parokia ya Mwenge katika Jimbo Kuu la Dar es Salaam na anatarajia kupewa Daraja Takatifu ya Upadri tarehe 25.04.2026 katika Parokia ya Mwenge Jimbo Kuu la Dar es Salaam.

Tumuombe ili aweze kufikia Daraja hiyo anayoitamani.

### **MASOMO YA DOMINIKA**

#### **DOMINIKA YA 3 YA KWARESIMA MWAKA A - TAREHE 08.03.2026**

SOMO I	Kut.17: 3-7
WIMBO WA KATIKATI	Zab 95: 1-2, 6-9
SOMO II	Rum.5: 1-2, 5-8
SHANGILIO	Yn.4:15
INJILI	Yn.4: 5-42

